# SERIKALI YA KAUNTI YA NAROK

S.L.P 898 - 20500, NAROK

## NOTISI KWA UMMA

## USHIRIKI WA UMMA KATIKA UTAYARISHAJI WA NAKALA YA MPANGO WA KIFEDHA WA KAUNTI (CFSP) NA MSWADA WA KIFEDHA WA KIPINDI CHA 2023/2024

Kufungamana na kanuni za Katiba ya Kenya ya 2010, Sheria ya Serikali za Kaunti ya 2012 na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma 2012 inayotaka pawepo uwazi na uwajibikaji, Serikali ya Kaunti ya Narok inawaalika wadau wote wanaojumuisha taasisi, mashirika yasiyo ya kiserikali katika sekta ya kibinafsi na watu binafsi, kuwasilisha mapendekezo kuhusu hatua za sera za kiuchumi zinazojumuisha mkakati wa uimarishaji wa mapato ya kaunti, ili yazingatiwe katika utayarishaji wa Nakala ya Mkakati wa Kifedha wa Kaunti ya Narok (CFSP 2023) na Mswada wa Fedha wa 2023. Ili kufanikisha mashauriano katika muda uliowekwa na uzingatiaji mwafaka wa masuala, mapendekezo yako yanapaswa yawasilishwe katika nakala ngumu kwa Hazina ya Kaunti ya Narok ili kufikia mpokezi aliyetajwa hapa chini kabla ya **tarehe 18 Februari 2023.** Nakala za kielektroniki zinapaswa kuwasilishwa kupitia barua pepe yetu: economicplanning@narok.go.ke

Wadau, kadhalika, wanashauriwa kuwianisha mapendekezo yao na nguzo kuu za maendeleo zilizo katika Ruwaza ya Ustawi wa Kenya ya 2030; sera za Kitaifa, Kikanda na Kaunti; rasimu ya CIDP III; Mpango wa Ustawi wa kila Mwaka; Ripoti za sekta miongoni mwa sera na mipango mingine husika. Maoni yanayowasilishwa yanapaswa kujumuisha mihimili tekelezi ya kuharakisha na kudumisha ukuaji jumuishi kwa minajili ya ustawi wa kijamii, kiuchumi na kimazingira. Zaidi ya hayo, maoni hayo yanapaswa kuwa bayana kuhusu mbinu zinazotakikana au masuala ya kushughulikiwa na yaeleze sababu wazi za kutolewa kwa mapendekezo hayo.

Aidha, wadau wote wanaalikwa kuhudhuria vikao vya umma **tarehe 18 Februari 2023** katika maeneo mbalimbali yaliyoonyeshwa hapa chini na ratiba yake.

| S/No. | Kaunti Ndogo | Mahali | Mada ya Mashauriano | Tarehe | Saa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Transmara West | Kilgoris Social Hall | Sector Proposals, CFSP & Finance Bill 2023 | 18.02.2023 | 10:00am |
| 2. | Transmara South | Word of Faith Church Lolgorian | Sector Proposals, CFSP & Finance Bill 2023 | 18.02.2023 | 10:00am |
| 3. | Transmara East | Emurua Dikirr Church of God | Sector Proposals, CFSP & Finance Bill 2023 | 18.02.2023 | 10:00am |
| 4. | Narok Central | Narok Youth Em-powerment Centre – Narok Town | Sector Proposals, CFSP & Finance Bill 2023 | 18.02.2023 | 10:00am |
| 5. | Narok North | Full Gospel Church, Olkurto | Sector Proposals, CFSP & Finance Bill 2023 | 18.02.2023 | 10:00am |
| 6. | Narok East | Nairegia Enkare Social Hall | Sector Proposals, CFSP & Finance Bill 2023 | 18.02.2023 | 10:00am |
| 7. | Narok South | Youth Empowerment Centre - Ololulunga | Sector Proposals, CFSP & Finance Bill 2023 | 18.02.2023 | 10:00am |
| 8. | Narok West | KAG Church Lemek | Sector Proposals, CFSP & Finance Bill 2023 | 18.02.2023 | 10:00am |

Tafadhali kumbuka kuwa kwa madhumuni ya maandalizi ya kutosha ya shughuli hii, nakala za kielektroniki za rasimu ya sera, mipango na miswada, zinaweza kupakuliwa kutoka kwa tovuti ya kaunti hii www.narok.go.ke huku nakala ngumu zikipatikana katika ofisi iliyotajwa hapa chini.

**WAZIRI WA KAUNTI (CECM) – FEDHA NA MIPANGO YA UCHUMI**
**SERIKALI YA KAUNTI YA NAROK**